TANGAZO LA SERIKALI NA. 661 la tarehe 8/9/2023

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA YA MIKOPO KUTOKA TAASISI ZA KIFEDHA ZA NJE KATIKA MRADI WA UJENZI NA UENDESHAJI WA KITUO CHA KUHIFADHI GESI NA UANZISHAJI WA VITUO VYA USAMBAZAJI KWA KAMPUNI YA TAIFA GAS TANZANIA
(KAMPUNI YA MIHAN GAS) YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio Kwenye Riba ya Mikopo Kutoka Taasisi za Kifedha za Nje Katika Mradi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Kituo cha Kuhifadhi Gesi na Uanzishaji wa Vituo vya Usambazaji kwa Kampuni ya Taifa Gas Tanzania (Kampuni ya Mihan Gas) ya Mwaka 2023.

Msamaha

2. Kodi yote ya zuio kwenye riba ya mikopo kutoka taasisi za kifedha za nje kwa ajili ya mradi wa ujenzi na uendeshaji wa kituo cha kuhifadhi gesi na uanzishaji wa vituo vya usambazaji, inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Taifa Gas Tanzania (Kampuni ya Mihan Gas), inasemehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 2 Julai, 2024 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Taifa Gas Tanzania (Kampuni ya Mihan Gas) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 25 Machi, 2022.

Dodoma,
25 Agositi, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*